

**OFISI YA RAISI
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHURI YA WILAYA YA IRINGA**



TANGAZO

**UKODISHAJI WA GHALA(KARAKANA) LA HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA
LILILOPO IPOGORO KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020-2021/2022**

TAREHE: 17/06/2019

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa anawatangazia Wafanyabiashara wote, Vikundi vilivyosajiliwa, Makampuni na Watu binafsi wenye uwezo na sifa za kukodi ghala (Karakana) la Halmashauri ya Wilaya Iringa lililopo Ipogoro kama ilivyo elekezwa kwenye jedwali hapa chini kwa kipindi cha mwaka fedha 2019/2020-2021/2022 kwa kuleta maombi yao:

NAMBA YA ZABUNI	ENEO ILIPO	MAELEZO
LGA/026/2019/2020/S/33	Ipogoro	Ukodishaji wa Ghala(Karakana) ya Halmashauri ya Wilaya Iringa

MASHARTI YA WAOMBAJI:

1. Kila mwombaji ni lazima awe raia wa Tanzania.
2. Muombaji aambatishe usajili wa TIN (au VAT)
3. Muombaji anatakiwa awe na Leseni husika.
4. Muombaji aambatishe uthibitisho wa ulipaji kodi (Tax Clearance Certificate) ya mwaka 2019/2020
5. Uthibitisho wa uwezo wa Muombaji kifedha kwa kuonyesha Taarifa ya Fedha ya Benki (Bank Statement) ya miezi mitatu ya hivi karibuni iliyo idhinishwa na kuthibitishwa na Meneja wa Benki ya tawi husika.

6. Muombaji aambatishe uhalali wa kisheria (Power of attorney) wa mtu atakaye husika na zabuni hii.
7. Taarifa ya madeni yake yote (kama yapo) anayo daiwa na watu binafsi, Benki na Halmashauri hii au nyingine katika Tanzania
8. Muombaji anatakiwa kutokuwa na mgogoro wowote na Halmashauri.
9. Muombaji atakayepata kazi atatakiwa awasilishe alipe/ (dhamana) fedha taslimu zinazolingana na mawasilisho ya miezi mitatu (3). Fedha hizi atarudishiwa baada ya mkataba kuisha endapo atakuwa hadaiwi.
10. Muombaji anatakiwa kulipa ada ya maombi ya Shilingi ishirini elfu tu (TZS. 50,000.00) kwa kila ombi la Mzabuni na kupewa stakabadhi pamoja na kabrasha la Zabuni ambalo utatakiwa kulijaza na kulirudisha kabla ya muda wa mwisho wa kupokea maombi. Ada ya maombi hairudishwi.
11. Maombi yafungwe katika bahasha kwa lakiri (Seal) katika bahasha mbili(2) moja halisi na moja nakala na kuonesha namba za zabuni, na kuwasilisha katika, **“OFISI YA KITENGO CHA MANUNUZI HALMASHAURI YA WILAYA IRINGA MAKAO MAKUU , S.L.P. 108, IRINGA”**
12. Maombi yaandikwe kwa, **KATIBU WA BODI YA ZABUNI, HALMASHAURI YA WILAYA IRINGA S.L.P. 108, IRINGA.**
13. Maombi ambayo hayatazingatia masharti ya kazi iliyotajwa hapo juu hayatafikiriwa.
14. Waombaji wote wanakaribishwa kufika wenyewe au kutuma wawakilishi wenu siku ya ufunguzi. Kwa maelezo zaidi wasiliana na Katibu wa Bodi ya Zabuni Halmashauri ya Wilaya Iringa.
15. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 24/06/2019 saa nne kamili asubuhi (4.00) na zabuni zitafunguliwa baada ya muda wa mwisho wa kupokea maombi katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya Iringa.

LUCY N. NYALU,
KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W),
HALMASHAURI YA WILAYA
IRINGA.